

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA

13 MEI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA – TAREHE 13 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

210. MHESHIMIWA EDWIN MGANTE SANNDA (KONDOA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kwa muda mrefu tumepigania kuboreshwa kwa maslahi ya Madiwani ikiwemo posho za Vikao na Serikali imekuwa ikisisitiza kuongeza mapato ili Halmashauri ziweze kuwalipa Madiwani vizuri

kadri ya uwezo, wito ambao umeitikiwa vizuri, mwezi Februari 2019 tumepokea barua toka TAMISEMI ikielekeza Madiwani walipwe posho za Vikao shilingi 40,000/= na si vinginevyo:-

Je, kwa nini Serikali isiachie Halmashauri kulipa posho kadri ya uwezo kama ambavyo msisitizo umekuwa toka awali.

211. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Fedha za kuchochea maendeleo ya Jimbo (CDCF) zimekuwa na msaada mkubwa katika kusaidia maendeleo Majimboni:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza viwango vya fedha za Mfuko huo ili kuleta ufanisi zaidi.

212. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali italeti fedha za *on call allowance* kwa Madaktari wanaofanya zamu hasa katika Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya ambavyo mapato yake ni madogo kwani

sasa ni zaidi ya miaka 2 fedha hiyo haijaletwa na Serikali.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

213. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Viongozi wa Kimataifa wanapofanya ziara Tanzania walikuwa wakifika Zanzibar na kuonana na Rais wa Zanzibar:-

- (a) Je, kwa nini katika siku za karibuni Viongozi hao wamekuwa wakiishia Tanzania Bara;
- (b) Je, ni Viongozi wangapi wa Kimataifa ikiwemo Marais ambao wamefanya ziara Tanzania katika kipindi cha 2016/2017 na nchi wanazotoka;
- (c) Je, kati ya Viongozi hao ni wangapi wamefika Zanzibar na wangapi hawakufika na kwa sababu gani.

WIZARA YA MAJI:

**214. MHESHIMIWA LATHIFAH HASSAN CHANDE
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-
Serikali iliahidi Mji wa Liwale kufanyiwa usanifu
wa mradi wa maji:-

- (a) Je, ni lini mradi huo uliofanyiwa usanifu utakamilika na kuanza kutoa huduma ya maji kwa Wananchi wa Liwale;
- (b) Je, ni Kata zipi zilizopo katika Wilaya ya Liwale ambazo zitanufaika na mradi huo wa maji.

**215. MHESHIMIWA VENANCE METHUSALAH
MWAMOTO (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya ujenzi wa Mabwawa ya maji ili kupunguza matatizo ya maji Wilaya ya Kilolo.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**216. MHESHIMIWA JUMA OTHMAN HIJA
(TUMBATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Miongoni mwa malengo ya Benki ya

TPB ni kupeleka huduma za kibenki kwenye maeneo ya Vijijini na maeneo ya pembezoni ambayo hayafikiwi na huduma hizo:-

Je, ni kwa kiasi gani lengo hilo limefikwa mpaka kufikia mwaka 2018.

217. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuwasaidia Wananchi walioweka amana zao katika Benki ya FBME.



WIZARA YA NISHATI:

218. MHESHIMIWA MARY DEO MURO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia Wananchi wa Kiluvya Madukani, Mwanalugali na Mikongeni ambao wamepisha ujenzi wa njia ya umeme.

**219. MHESHIMIWA AGNES MATHEW MARWA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-
Nyumba nyingi za Vijijini hazikuwekewa umeme
wakati wa usambazaji japo baada ya kuweka
umeme kumekuwa na ongezeko la ujenzi wa
nyumba na uzalishaji mali kama ujasiriamali:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha
nyumba zote zilizobaki zinapata umeme kabla
mradi wa REA haujamaliza muda wake.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya
Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi
na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
13 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**